# Nadharia za Uhakiki kama Mchakato wa Kutaalamisha Usomaji wa Fasihi

*Richard M. Wafula*[*]

**Ikisiri**
*Utunzi na uhakiki wa fasihi ya Kiswahili umepanuka sana katika miongo mitano iliyopita. Makala haya yananuia kuonyesha dhima ya nadharia katika kutaalamisha usomaji wa fasihi. Nadharia za uhakiki (na wakati mwingine za utunzi) zimepevusha usomaji na uhakiki kwa viwango ambavyo havingeweza kukadirika hapo awali. Kwa njia hii, lugha ya Kiswahili imeweza kueleza maarifa anuwai kwa viwango vya juu. Nadharia na mikondo ya uhakiki kama usemezano na udenguzi vimetuwezesha kuchanganua matini ya kifasihi kwa jicho la upekuzi. Kwa upande mwingine, changamoto katika utumiaji wa baadhi ya nadharia hizi zimejitokeza na zinapaswa kutathminiwa katika mazingira ambamo lugha ya Kiswahili inaendelea kutumiwa kufafanulia ujuzi wowote ule. Makala haya yanatalii manufaa ya matumizi ya nadharia katika uhakiki na kuweka wazi matatizo yanayoandamana na matumizi ya baadhi ya nadharia hizo. Hatimaye, njia mwafaka ya kufuatwa imependekezwa.*

**Dhana za msingi:** *utunzi, uhakiki, fasihi ya Kiswahili, nadharia za uhakiki*

**Abstract**
*The authorship and criticism of Kiswahili literature has expanded exponentially in the last five decades. This article intends to show the role of theory in professionalizing the reading of the literature. Critical theories (and sometimes creative ones) have deepened and enriched reading and criticizing Kiswahili literature to levels that had not been contemplated previously. In this way, Kiswahili has been able to express diverse and sophisticated ideas. Theories and literary currents such as dialogism and deconstructionism have facilitated careful and systematic analysis of Kiwahili literary texts. On the other hand, the proliferation of so many theories have been replete with challenges associated with relevance and adaptability in a context in which Kiswahili is increasingly becoming a vehicle for elaborating any type of knowledge. The article explores advantages of using theory to inform criticism and also lays bare problems faced in applying some of them. Finally, the way forward is proposed.*

**Keywords:** *authorship, criticism, Kiswahili literature, critical theories*

[*]Lecturer, Department of Kiswahili and African Languages, Kenyatta University, P.O. Box 43844, Nairobi 00100, Kenya, E-mail: rnamwinguli@gmail.com

## Utangulizi

Ni ukweli usiopingika kwamba lugha na fasihi ya Kiswahili vimeshughulikiwa tangu karne ya 19 na wataalamu wa Kimagharibi kama Edward Steere (1870), Alice Werner (1933), W. Hichens (1939, Carl Velten (1955), na Jan Knappert (1979). Wataalamu hawa walitumia nadharia zilizojikita katika utamaduni wa Waswahili na Waafrika wengine kwa ujumla kufanya tafiti zao. Hata hivyo, uandishi na usomaji wa fasihi ya Kiswahili umepanuka sana katika miongo mitano iliyopita kwa namna ambayo haingeweza kukadirika hapo awali. Kabla ya mwaka 1990, uhakiki wa fasihi ulielekezwa katika usomaji makini wa ushairi, tamthilia, na riwaya mbalimbali katika ufundishaji wa wanafunzi wa shahada ya kwanza wa vyuo vikuu na wale wa shule za sekondari. Kwa upande wa uhakiki katika kiwango cha uzamili, jitihada za kuzingatia vipengele vya nadharia katika tafiti zilizofanywa zilikuwapo. Hata hivyo, kwa ujumla, ingawa wahakiki walioongozwa na mielekeo na mitazamo ya kinadharia kutoa kauli zao, mielekeo na miongozo hiyo ilifumbatwa katika msamiati na maoni binafsi ya mhakiki. Ulikuwa wakati ulioficha uwazi wa nadharia katika uhakiki. Kilichokaribia nadharia ni kitengo kilichohusu falsafa ya mwandishi. Tahakiki za mwanzomwanzo, kama *Ndimi Zetu* (1974), *Hisi Zetu* (1973), *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili: Kitabu cha Kwanza* (1971), *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili: Kitabu cha Pili* (1977), na *Ushairi wa Shabaan Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake* (1974), zilihusu na zinawakilisha aina hii ya uhakiki wa fasihi. Vilevile, tangulizi za Shihabuddin Chiragdin katika diwani za *Malenga wa Mvita* (1970), *Malenga wa Mrima* (1977), na *Sauti ya Dhiki* (1973) zilichangia uhakiki wa fasihi.

## Nadharia Zajitokeza

Nadharia zilianza kujitokeza kwa uwazi katika makala ya Kahigi na katika tangulizi zilizoandikwa na Kahigi na Mulokozi (1979, 1995). Makala ya Kezilahabi (1983), Kitabu cha Senkoro (1987), dibaji za Abdilatif Abdalla Katika *Diwani ya Jinamizi* (1977), na *Diwani ya Nyamaume* (1976) ni baadhi ya kazi zilizochangia chanzo cha nadharia za uhakiki kama taaluma inayojisimamia. Mwelekeo wa kinadharia uliojitokeza ni wa Elimu-jamii, hususan wa Kimarx au wa uhalisia wa kijamaa. Athari za wataalamu wa siasa, historia, elimu-jamii, na saikolojia ya ukoloni, kama Frantz Fanon, Amilcar Cabral, Mwalimu Julius K. Nyerere, na Walter Rodney, na watunzi wa mtazamo wa kimapinduzi, kama Ngugi wa Thi'ongo, Sembene Ousmane, Alex La Guma, na Agostinho Netto, zilihamasisha na kurutubisha matumizi ya nadharia ya Umarx na uhalisia wa kijamaa. Isitoshe, katika miongo ya sitini hadi ya tisini ya karne iliyopita, harakati za ukombozi katika kanda ya kusini ya bara la Afrika zilipata ufadhili kutoka kwa mataifa ya mrengo wa kushoto wa wakati huo. Mataifa kama Cuba ya Fidel Castro, uliokuwa Muungano wa Usovieti wa Nikita Kruschev na Leonid Brezhnev, na Uchina chini ya uongozi wa Mao tse Tung yalichangia kwa kiasi kikubwa kuratibu itikadi za kisiasa barani. Itikadi hizi na mawazo ya viongozi hawa vilipalilia uandishi na uhakiki ulioegemea mtazamo wa Kimarx. Huu ulikuwa wakati wa kuanguliwa kwa mawazo mazito yenye mwelekeo wa kinadharia na hauwezi kupuuzwa kamwe tunapofikiria juu ya uundaji wa nadharia katika nyanja mbalimbali za utaalamu wa Mwafrika, fasihi ya Kiswahili ikiwemo.

Kama ilivyotajwa hapo awali, nadharia zilikuwa tayari zimeshindilia mizizi yake katika kiwango cha uzamili. Katika nchi ya Kenya, Jay Kitsao (1975, 1982), Kazungu Kadenge (1982), na Chacha Nyaigotti Chacha (1980, 1987) ni miongoni mwa watafiti wa kwanza wa fasihi ya Kiswahili kutumia nadharia kwa uwazi katika uhakiki wa matini zao. Nchini Tanzania, kutokana na maandishi na insha za Shaaban Robert na utunzi na uhakiki wa Euphrase Kezilahabi, ilikuwa wazi kwamba riwaya ya kitasinifu ilikuwa imeshindilia mizizi yake. Mapema kabla ya uhuru wa kisiasa kupatikana katika kanda ya Afrika Mashariki, Shaaban Robert alikuwa amebashiri kwamba ufukara, ugonjwa, kutojua kusoma na kuandika, na ukosefu wa ajira ndizo zingekuwa changamoto kuu za nchi zilizokuwa zikipigania uhuru.

Ebrahim Hussein na Kezilahabi, mwishoni mwa mwongo wa sita na mwanzoni mwa mwongo wa saba wa karne ya 20, walikuwa wameshatambua kwamba matumaini ya Mwafrika katika kukabiliana na ujinga, ugonjwa, na ufukara yalikuwa yamezikwa katika kaburi la sahau. Maandishi yao yalitokana na halisi ya maisha ya wakazi wa Afrika Mashariki na upwa wake. Yaani, wawili hao walikuwa wamethibitisha utabiri wa Shaaban Robert. Kazi za S. A. K. Mlacha na J.S. Madumulla pia ziliwaauni wanafunzi na wahakiki kufikiria kuhusu kutaalamisha usomaji wa fasihi. Ijapokuwa nadharia ya Kimarx katika viwango anuwai vya ufasiri iliendelea kutamalaki katika ulingo wa uhakiki, nadharia nyingine, hasa za kimtindo na za kisaikolojia, zilikuwa zikibisha hodi kwa kishindo. Kwa ujumla, kufikia mwaka 1990, nadharia za uhakiki zilikuwa zimeanza kushughulikiwa kama kozi zinazojisimamia katika viwango mbalimbali vya mafanikio katika vyuo vikuu. Hivi sasa, takriban vyuo vyote katika kanda ya Afrika ya Mashariki vinafundisha nadharia za uhakiki wa fasihi. Nao wahakiki walijitwika mzigo wa kuandika tahakiki kwa mwelekeo wa kinadharia. Miongoni mwa wahakiki hao walikuwa Mbunda Msokile (1995), Kimani Njogu na Rocha Chimerah (1999), Kyalo Wamitila (2002, 2003, 2008), na R.M. Wafula na Kimani Njogu (2007).

**Manufaa ya Nadharia za Uhakiki wa Fasihi**

Ufundishaji wa nadharia za uhakiki ulileta manufaa mengi. Manufaa ya wazi sana ni kwamba nadharia za uhakiki kama taaluma zilipanua mawanda na upeo wa usomi wa wanafunzi, waalimu, na wataalamu wengine wa fasihi. Pamoja na kudurusu riwaya, tamthilia, na ushairi, wahadhiri wa vyuo vikuu walianzisha kozi zilizojisimamia juu ya nadharia za uhakiki wa fasihi. Miongoni mwa nadharia hizo, zile zilizohusu mikondo mbalimbali ya kukua na kusambaa kwa fasihi zilikuwa mashuhuri zaidi. Nadharia kama urasimi, urasimi-mpya, ulimbwende, uhalisia, udhanaishi, umaumbo, na umuundo ni baadhi yake. Somo la fasihi simulizi lilipoanza kushughulikiwa lilizua maswala kinadharia vilevile. Nadharia ya kiutanzu na nadharia zinazofafanua ubunifu na uwasilishaji wa tanzu mbalimbali zikaanza kufikiriwa kwa kina zaidi. Kwa kifupi, baadhi ya nadharia ziliweka na zinaendelea kuweka wazi baadhi ya kadhia za kifasihi.

Isitoshe, nadharia nyingi miongoni mwa zile zilizofundishwa zilitokana na wataalamu wa Kimagharibi. Zilihitaji kutafsiriwa kwa namna inayoeleweka kwa urahisi. Mhadhiri wa nadharia za uhakiki alijikuta amejitwika jukumu jingine. Jukumu hilo lilikuwa la mtafsiri wa dhana na maelezo ya kinadharia. Majarida ya *Kiswahili*, *Mulika,* na *Kioo cha Lugha* yamekuwa yakitumiwa kukusanya na

kutafsiri baadhi ya istilahi hizo. Majarida haya yamewakabidhi wasomi msamiati wa kimsingi wa kufundishia nadharia za uhakiki wa fasihi. Mwaka 1989, nilipofundisha nadharia za uhakiki wa fasihi kwa mara ya kwanza, nilikabiliana na istilahi "Romanticism". Mwaka huo nilitafuta kisawe cha Kiswahili nisikipate. Kwa hiyo, niliitafsiri istilahi hiyo, nikishirikiana na Mutegi Mukobwa, kama "udhahania nafsia", neno ambalo tuliliacha mara tu tulipoliona neno "ulimbwende" kutoka katika kitabu cha Senkoro (1987).

Nadharia za uhakiki zimewawezesha wahadhiri wa fasihi kuuweka uhakiki katika utaratibu maalumu. Utaratibu huo umechukua umbo la mtazamo wazi. Pale ambapo uhakiki ulishughulikia mazingira ya mwandishi, maudhui, wahusika, na matumizi ya lugha, hivi sasa nadharia imeingiza kipengele cha ushahidi unaotokana na mtazamo wa msomaji unaojulikana na kaumu ya wasomaji wengine katika usomaji. Udadisi wa mhadhiri sasa unafuata mikakati mahsusi ya uhakiki wa kazi za fasihi. Kwa kufanya hivyo, somo la fasihi limepewa silaha za kiakademia na kuanza kusheheni sifa za kitaalamu. Silaha hizi ni mbinu za uhakiki na msamiati wake. Vilevile wahakiki wamepewa uwezo wa kukadiria kupata matokeo yaleyale iwapo watatumia mbinu na miongozo inayoshabihiana kutathmini kazi moja. Kwa kiwango kikubwa nadharia za uhakiki zimehamasisha usanifishaji wa ufundishaji wa fasihi katika vyuo vikuu. Kazi kama *Mwisho wa kosa* (1987) na *Cheche za Moto* (2008) zinashabihiana kwa kutumia baadhi ya mitazamo ya kinadharia. Nadharia nyingine kama umuundo zinaweza kutumiwa kuzilinganua riwaya hizo. Jambo muhimu ni kwamba riwaya hizi zinaweza kulinganishwa na kulinganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia zinazoelezeka kinagaubaga.

Hapo awali uhakiki aghalabu ulishirikisha jumla ya mawazo binafsi kuhusu kazi inayochanganuliwa na pengine mawazo hayo yangehusishwa na nadharia isiyotambulika kinaganaga. Nadharia za uhakiki zimezalisha ufasiri wa kutegemewa wa kazi za fasihi. Kutokana na jambo hili, mhakiki amesaidiwa kuyachuja makisio yake kuhusu kazi inayohakikiwa na kubaini iwapo makisio hayo yatabakia kuwa makisio au yatageuzwa kuwa ujuzi wa kutegemewa. Pamoja na nadharia zinazohusu mikondo na nyakati kama udhanaishi, uhalisia, urasimi, uhalisia wa kijamaa, urasimi-mpya, ubwege, nadharia ya kiutanzu, na mwitikio wa msomaji, baadhi ya nadharia za kimtindo kama ya vikale na ya ubayana au uchimuzi zimefanikiwa kuwakabidhi wahakiki msimbo wa kutaalamisha eneo lao la usomi.

Kwa kifupi, nadharia zimeshadadia kuwafikirisha wasomi wa fasihi kisayansi. Kazi za fasihi anuwai zinaweza kutazamwa kwa mujibu wa mihimili ya nadharia moja. Katika muktadha huu, nadharia imekuwa kama mkakati wa kuzikagua kazi hizo za fasihi. Nadharia vilevile zimekuwa kama kichocheo cha utafiti mpya kwa kujaribiwa katika miktadha mbalimbali. Baadhi ya nadharia zimebidika kunyambuliwa au kutumiwa kiuchangamano ili zichanganue malighafi mahsusi na za kipekee. Katika fasihi simulizi za Kiafrika, kwa mfano, mitazamo ya kietiki inapaswa kutumiwa sawia na mitazamo ya kiemiki ili matokeo ya uchanganuzi yawe ya kufana na kutegemewa. Mitazamo inayoeneza mielekeo hasi na kibaguzi kama ya G. F. Hegel na David Hume inaweza kusailiwa na kusambaratishwa kupitia nadharia pinzani na yenye mashiko katika ukweli.

Hatimaye, kwa kutumia nadharia, wafafanuzi wa fasihi wameunda usemaji ambao umewawezesha kushindana na wataalamu wanaopatikana katika mawanda mengine ya usomi. Katika zama zetu, bila kuunda usemaji wenye mamlaka ya kuweza kuwanyamazisha wengine wanaoshindana na wasomi wa fasihi, wasomi wa fasihi watamilikiwa abadan na wataalamu wa nyanja nyingine. Ikiwa madaktari, wahandisi, wanabaiolojia, na wanahewa wana misimbo yao na lugha yao ya kipekee, iweje wahakiki wasiwe na msimbo wao usioeleweka na wengine. Utabaka katika hali hii ni chanya; si hasi. Ni utabaka unaomtenga mja kitaalamu. Nadharia za uhakiki zimeongeza fahari juu ya usomi wa fasihi kwa kuutaalamisha ugo huo wa ujuzi. Zimewawezezesha wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kuizungumzia fasihi kwenye majukwaa ya kimataifa.

**Changamoto za Kutumia Baadhi ya Nadharia**

Wahenga wanasema hakuna masika yasiyokuwa na mbu. Ufundishaji wa nadharia za uhakiki wa fasihi umekumbwa na changamoto kochokocho. Kwanza, kwa kuwa nadharia nyingi zinazofundishwa zimeazimwa kutoka kwa wataalamu wa Kimagharibi, kila msomi hutafsiri istilahi za kinadharia kivyake. Istilahi kama 'urasimi' na 'urasimu', 'uumbuzi', 'ujenguzi', 'udenguzi', 'usemezo', na 'usemezano' zimesababisha kuchanganyikiwa kwingi miongoni mwa wanafunzi na wasomi wa fasihi. Mbali na haya, msamiati wa kiuhakiki uliotoholewa kutoka lugha ya Kiarabu kama 'jazanda', 'istiari', ' istiara', 'stiari', 'taswira' na 'taashira', na 'ishara' umezusha utata si haba. Tatizo hili litasuluhishwa iwapo tutakuwa na vikao vya kusanifisha istilahi na msamiati unaotumika katika taaluma ya nadharia za uhakiki wa fasihi. Katika mazungumzo ya kawaida, hakuna haja ya kuwalazimisha watu kutumia mtindo mmoja. Lakini katika utaalamu wa fasihi au utaalamu wa aina yoyote wataalamu wanapaswa kutumia lugha inayoeleweka kati yao.

Isitoshe, nadharia zimeibuka kuwa utanzu unaojisimamia na kujitosheleza kufundishwa katika baadhi ya vyuo vikuu badala ya kuwa sehemu ya uhakiki. Kutokana na jambo hili, baadhi ya nadharia hufundishwa bila jaribio la kuonyesha ufaafu wake katika uhakiki wa fasihi, hasa uhakiki wa kazi za Kiswahili. Tatizo hili limekithirishwa na nadharia za kisasa (kama umuundo) na nadharia za kisasaleo (kama udenguzi) zinapoingia katika uhakiki wa fasihi. Nadharia hizi hazikushughulikia mada za uhakiki wa fasihi moja kwa moja na pale zilipotumiwa katika uhakiki ziliichana kazi ikabaki bila thamani yoyote, ikawa kama tapu la muwa, kokwa la embe au ganda la ndizi. Kwa muhtasari, nadharia zilijilenga zenyewe badala ya kulenga matini chasili za fasihi. Swala la usanii katika fasihi lilipuuziliwa mbali, uhakiki ukawa ni mchezo wa maneno usiokuwa na lengo la kuiboresha kazi ya fasihi au mtunzi mwenyewe.

Ili nadharia ya uhakiki iwanufaishe watumiaji wake, inapaswa kutumia nguzo zake kufafanua vielezi vya dhana ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Kwa mfano, kielezi cha moja kwa moja cha fasihi ni:

> Fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa na huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani (Wamitila, 2002:13).

Nadharia ya uhakiki wa fasihi mwafaka inapaswa kumsaidia msomaji kufahamu kielezi hiki cha fasihi. Msomaji anatarajia kufahamishwa jinsi nadharia fulani inavyofafanua 'fasihi', 'sanaa', 'lugha', na 'umbo'. Maneno 'fasihi' na 'sanaa' ni ya kidhahania. Nadharia ya uhakiki itamfaidisha msomaji ikiwa itatoa mwongozo kuhusu ufafanuzi wake. Nadharia za urasimi na uhalisia zinajaribu kumwelekeza msomaji katika kuelewa maana ya maneno hayo. Lakini, tukichukua nadharia za umuundo na udenguzi na kujiuliza: je, nini madai ya nadharia hizi kuhusu maana ya fasihi, dhima ya fasihi katika jamii, na namna mbalimbali za kutenganisha sanaa bora kutokana na sanaa chapwa? Hatutapewa jawabu la kutegemewa. Hii ina maana kwamba mhakiki hawezi kutumia nadharia kama hizi kuimarisha viwango vya kutegemewa vya ubora wa uhakiki. Hatuwezi kukadiria thamani ya fasihi kutokana na madai yake. Katika udenguzi mhusika hawezi kuwa kielelezo chochote kwa sababu, kabla kielelezo hicho kutengemaa, kitajiumbua chenyewe. Mhusika yuleyule akichanganuliwa katika muktadha wa umuundo atakuwa kifaa chenye dhima ya kufanikisha masimulizi ya mtambaji au msimulizi. Ni moja kati ya samani zinazoyasukuma masimulizi mbele. Nadharia hizi zinapotumiwa na mhakiki, mhakiki anapaswa kujihadhari kuhusu ufaafu wake. Kinyume na haya, nadharia kama ufeministi inapokabiliana na mhusika katika kazi ya sanaa, mhusika huyo anawakilisha binadamu ambaye ana mtazamo na mielekeo maalumu ambayo kwayo msomaji anaweza kuhitamidi ujuzi fulani hata kama hakubaliani na misingi yake kinadharia.

Imebainishwa awali kwamba nadharia bora inapaswa kuwa na manufaa kwa mtumiaji wake. Manufaa ya baadhi ya nadharia za kisasaleo ni kumfikirisha msomaji katika mizunguko na malumbano yasiyokwisha. Tunaposonga mbele na kukaribisha nadharia mpya na za kigeni tunapaswa kufikiria pia juu ya ufaafu wake. Tunaweza kufanya hivyo kwa kuzifinyanga ili ziendane ipasavyo na ufafanuzi wa fasihi na muktadha wa Kiafrika. Nadharia ya ufeministi, kwa mfano, imenyambuliwa na kuunda ufeministi wa Kiafrika kuafikiana na mazingira ya bara la Afrika. Lakini swala lote kuhusu nadharia za uhakiki linaweza kufikiriwa upya kwa kuendeleza juhudi zilizoanzishwa na watangulizi wetu.

**Tufikirie Upya Kinadharia**

Kuna insha zilizoandikwa zamani kuhusu uhakiki wa fasihi na waandishi kama Shaaban Robert, Shihabuddin Chiragdin, Abdilatif Abdalla, Said Ahmed Mohamed, Ebrahim N. Hussein, Euphrase Kezilahabi, Penina Mlama, Hassan Msami, Joshua Madumulla, na shaaban Mlacha zinazoweza kusomwa na kupewa uzito wa kinadharia. Isitoshe, tahakiki za waandishi wa Kiafrika kama Wole Soyinka, Chinua Achebe, Ngugi wa Thiong'o, Ezekiel Mphalele, Ama Ata Aidoo, Ifi Amadiume, Micere Mugo, Okot P'Bitek, na Leopold Sedar Senghor walioandika na wengine wanaoendelea kuandika katika lugha za kigeni yanaweza kuhusishwa katika mchakato wa kufikiria upya kuhusu nadharia za uhakiki. Insha za Amilcar Cabral katika chapisho lake mashuhuri *Unity and Struggle* (1980), kwa mfano, zinaibua masuala ya uhalisi katika harakati za kujikomboa, jinsi ya kukabiliana na utamaduni unaokengeusha, umuhimu wa uadilifu, usawa wa kijinsia, na haki za watoto na vijana kwa uasili na ubunifu unaosisimua mtima na kuhekemiza na kuridhisha ubongo. Inapendekezwa ya kwamba machapisho kama haya yasomwe na wanafunzi wa fasihi za Kiafrika.

Nadharia kama jumla ya mawazo au dhana zinazotolewa ili kufafanua hali fulani hazitoki angani. Huundwa na wanajamii kama hawa niliowataja. Mawazo yao yakapanuliwa na kukuzwa na waitifaki kama sisi. Hivi leo taarifa nyingi za fasihi simulizi na fasihi andishi zipo. Kufikia mwaka 2010 tamthilia na riwaya zaidi ya 2000 zilikuwa zimeandikwa katika lugha ya Kiswahili (Zubkova, Gromov, Khamis & Wamitila, 2009). Kutokana na kuzichunguza zenyewe, tunaweza kuunda nadharia za utunzi na pia za uhakiki. Huu si muujiza kwa vile nadharia si chochote bali vigezo vinavyotusaidia kuhakiki vilivyoundwa kitambo au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo linalohusika lenyewe.

Umajazi na ujalizaji unaweza kuchunguzwa kama mkakati unaowangoza waandishi na wahakiki wa sampuli maalumu za tungo za Kiswahili. Kutokana na udurusu wangu wa masimulizi na maigizo yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili, imebainika kwamba majazi hutumiwa katika viwango mbalimbali katika ufasiri wa kazi ya fasihi (Wafula, 1989). Mwandishi aliyevitumia viwango vingi vya majazi alikuwa Shaaban Robert. Hata hivyo, katika masimulizi yake ya mwishomwisho, matumizi ya majazi yalielekea kufifia, akaanza kutumia mtindo wa uyakinifu. Mtindo huu unaokaribiana na uhalisi wa maisha ulirithiwa na watunzi wengi walioanza kutunga na kuchapisha katika miaka ya sabini. Lakini mtindo wa awali wa Kishaaban haukutokomea kabisa. Umechipuka katika kazi za Kezilahabi kama *Nagona* (1990) na kazi za Katama Mkangi kama *Walenisi* (1995).

Kutokana na haya, baadhi ya kazi za Kiswahili zinaweza kusomwa kuwili kulingana na mwelekeo na kiwango cha ujalizaji wa majazi. Mhakiki atakuwa na jukumu la kuainisha na kuchanganua viwango mbalimbali vya majazi kuweka wazi maana ambazo zinajitokeza kutokana na viwango hivyo. Ikiwa riwaya au tamthilia ni ya kimajazi moja kwa moja, ufasiri wake utalenga katika kufafanua na kuziweka wazi maana na viashiria mbalimbali vya kimajazi. Kwa upande mwingine, ikiwa riwaya au tamthilia inaelekea kuafikiana na hali yakinifu ya maisha, mhakiki atajaliza vilevile kwa kufasiri maana mbalimbali zinazojitokeza kutokana na usimulizi ulio mbele yake. Kwa vyovyote vile, msomaji hawezi kuepuka umajazi au ujalizaji anapokumbana na kazi ya fasihi ya Kiswahili. Riwaya za mwanzo za Shaaban Bin Robert zinafungamana na matumizi ya majazi ya kimapokeo. Nayo riwaya ya Suleiman Mohamed *Nyota ya Rehema* (1978) inaweza kufasiriwa kimajazi kwa kusema kwamba riwaya hiyo inawahekemiza wasomaji wake kuwa "haki ya mtu haipotei"

Kwamba Waswahili hawana mtu anayeitwa Plato au Aristotle katika mapokeo yao haina maana kwamba hawana fikra za kijumuia zinazoshabihiana au nzuri zaidi kuliko za Plato na Aristotle. Muyaka Bin Haji, Ali koti, Mwanakupona, Mataka na Nassir walifikiria kuhusu uigo kama mbinu ya kusanifu na kusarifu tungo za sanaa. Baadaye, Amri Abedi, Shaaban Robert, Shihabuddin Chiragdin, na Mathias Mnyampala wakauliza maswali juu ya maana ya ushairi, dhima ya ushairi na jinsi ya kuainisha tungo mufti kutokana na tungo chapwa. Huku kulikuwa kufikiria kinadharia. Tujenge minara mirefu zaidi kutokana na watangulizi hawa.

Mdurusu yeyote anaposoma insha za Shihabuddin Chiraghdin kuhusu jinsi mashairi ya Kiswahili yanavyopaswa kupokelewa na kuitikiwa hana budi kugundua kwamba kile anachoshughulikia Chiraghdin hasa ni nadharia ya kiutanzu.

Chiragdin anaanza ziara yake kwa kung'amua kwamba washairi wa Kiswahili wanatambua umuhimu wa arudhi. Lakini jambo ambalo limesemwa na wahakiki wachache ni kwamba Chiragdin hakwamii pale; anayagawanya mashairi ya Ahmad Nasir katika makundi manne: Mbinu za Lugha, Mawazo na Maliwazo, Baina ya Mume na Mke, na Majonzi na Makiwa. Ijapokuwa kuna utelezi mwingi katika uainisho huu, Chiragdin anatoa ithibati madhubuti kwamba mashairi ya Kiswahili yanaweza kugawanywa kimaudhui au kwa mujibu wa mada zinazoshughulikiwa. Abdilatif Abdalla anafuata mkondo unaokaribiana na Shibuddin Chiraghdin anapoandika utangulizi wa *Diwani ya Ustadh Nyamaume*. Anabainisha migawanyo sita ya mshairi: Kuusemea Ushairi, Malimwengu, Kushauri na Kunasihi, Kuimbana Kishairi, Kufumba na Kupiga Mifano, na Kushangilia na Kutoa Heko. La mno ni kwamba Abdalla amepanua kidogo matamko ya Chiraghdin ili atilie maanani upeo wote wa mashairi aliyoyatunga Nyamaume. Haya ni tofauti na anayoyafanya Hassan Msami katika kitangulizi chake cha *Malenga wa Vumba*. Anasisitiza zaidi uainisho wa kimuundo kwa kuwa mtunzi mwenyewe alikuwa akijaribia usemaji wa kishairi kimuundo. Miongoni mwa miundo anayoainisha ni kikai, msuko, sakarani, mtiririko, ukara, ukaraguni, kikwamba, msuko wa kikai, tathlitha, tarbia, takhmisa, ukemi, pindu, na utenzi. Jambo hili linayakinisha kwamba uainisho hutegemea kile ambacho mwainishaji anataka kutilia nuru. Kwa ujumla, fikra za waandishi wa tangulizi za diwani za mashairi zinaweza kutuauni kuwaza na kuwasilisha upya utaratibu wa uhakiki wa ushairi wa Kiswahili.

Ni jambo lisilopingika kwamba utandawazi uko nasi. Hata hivyo, tunapoupiga pambaja, inatupasa tukumbuke kwamba utandawazi huanzia katika kijiji fulani mahsusi. Yaani ubia na upekee hauwezi kutenganishwa kabisa. Ubia wa mapinduzi ya kisayansi na nadharia kwa ujumla ulisailiwa na si mwingine bali Mmagharibi anayeitwa Thomas Kuhn (1962, 2005). Kuhn alikatikiwa kung'amua kwamba mapinduzi ya sayansi na nadharia hutekelezeka katika muktadha wa utamaduni maalumu.

**Hitimisho**

Katika makala haya nimeonyesha jinsi nadharia zilivyoingia katika ufundishaji wa fasihi na kutaalamisha somo hilo. Pia nimeonyesha kwamba baadhi ya nadharia husababisha kuchanganyikiwa badala ya kumwauni msomaji kufafanua matini anayosoma. Nimependekeza kwamba inafaa kila inapohitajika kunyambua nadharia ya kigeni ili iendane ipasavyo na mazingira yanayohusika. Isitoshe, nimewashauri wahakiki kwamba kuna haja ya kusoma upya insha za wataalamu wa fasihi ya Kiswahili na wataalamu wa fasihi za Kiafrika, kuzikuza ili ziimarike kama nadharia. Vilevile, tunaweza kuunda nadharia kutokana na kazi za sanaa zilizoandikwa katika Kiswahili. Hatimaye, nitachelea kuziweka baadhi ya nadharia za kisasa na kisasaleo kwenye silabasi yangu chuoni.

**Marejeo**

Abdalla, A. (1976). Utangulizi wa Mhariri. Katika S. C. Gonga (mh.). *Diwani ya Nyamaume* Nairobi: Shungwaya Publishers.

Abdalla, A. (1976). Utangulizi wa Mhariri. *Diwani ya Jinamizi* (Salim Zakwany). Nairobi: Shungwaya Publishers.

Abedi, A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Achebe, C. (1988). *Hopes and Impediments.* London: Heinemann.

Asante, M. (1987). *The Afrocentric Idea*. Philadhelphia: Temple University Press.

Carby, H. (1996). White Woman Listen! Black Feminism and the Boundaries of Sisterhood. Katika B. D. Houston & R. Lindeborg (wah.). *Black British Cultural Studies: A Reader*. Chicago & London: The University of Chicago Press.

Cabral, A. (1980). *Unity and Struggle*. London: Heinemann.

Chacha, N. C. (1980). Ushairi wa Abdilatif Abdalla. Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi.

Fanon, F. (1977).*The Wretched of the Earth* (trans. Constance Farrington) Newyork: Grove Press.

Gikandi, S. (1987). *Reading the African Novel*. Nairobi: Heinemann.

Hichens, W. (mh.). (1939). *The Soul's Re-Awakening*. London: Sheldon Press.

Hussein, E. (1983). Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle, *Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Irele, A. (1982). *The African Experience in Literature and Ideology*. London: Heinemann.

Irele, A. (1964). A Defence of Negritude. *Transition*, 13(9-11).

Kazungu, K. (1982). Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Texts. Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi.

Kezilahabi, E. (1983). Uchunguzi katika Ushairi. *Fasihi.* Dar es Salaam: TUKI.

Kezilahabi, E. (1990). N*agona*. Dar es Salaam: DUP.

Kitsao, J. (1982). An Investigation of Themes in Swahili Literature and Application of Stylostatistics to Chosen Texts. Unpublished PhD Thesis, University of Nairobi.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse.* London: Heinemann.

Kuhn, T. (1962, 2005). *The Structure and Necessity of Scientific Revolution.* Chicago: University of Chicago Press.

La Guma, A. (1973). *In the Fog of the Season's End.* London :Heinemann.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Phoenix.

Mkangi, K. (1995). *Walenisi.* Nairobi: EAEP.

Mlama, P. (1983). Utunzi wa Tamthilia Katika Mazingira ya Tanzania. *Fasihi.* Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S. A. K. (1991). *A Linguistic Study of the Novel*. Berlin: Schreiber.

Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (2005). Signs of New Features in the Swahili Novel. *Research in African Literatures*, 36(1). Bloomington: Indiana University Press.

Mohamed, S. A. (1999). Towards Defamiliarization and Experimentation: Kezilahabi's Novel, *Nagona,* and the Future of Swahili Literature. Seminar Paper Read in Kisumu.

Mohamed, S. (1976). *Nyota ya Rehema.* Nairobi: Oxford University Press.

Mnyampala, M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: EALB.

Msami, H. (1982). Utangulizi, *Malenga wa Vumba* (Boukheit Amana). Nairobi: Oxford University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mulokozi, M. M. & Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. & Kahigi, K. K. (1995). *Malenga wa Bara*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwai, W. (1988). New Trends in Ushairi, Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi.

Njogu, K. (1997). *Mwongozo wa Amezidi*. Nairobi: Longhorn.

Njogu, K. & Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyerere, J. K. (1968). *Freedom and Socialism: A Selection from Writings and Speeches, 1965-1967.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (1979). *Crusade for Liberation.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Ousmane, S. (1960). *God's Bits of Wood.* London: Heinemann.

Rodney, W. (1972). *How Europe Underdeveloped Africa*. Dare es Salaam: Tanzania Publishing House.

Sengo, T. S. Y. & Kiango, S. D. (1973). *Hisi Zetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Sengo, T. S. Y. & KIango, S. D. (1974). *Ndimi Zetu.* Dar es Salaam: Press & Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press & Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Press & Publicity Centre.

Shihabuddin, C. (1970). Utangulizi, *Malenga wa Mvita* (Ahmad Nassir). Nairobi: Oxford University Press.

Shihabuddin, C. (1977).Utangulizi, *Malenga wa Mrima* (Mwinyi Hatibu Mohammed). Nairobi: Oxford University Press.

Soyinka, W. (1993). *Art Dialogue and Outrage: Essays on Literature and Culture*. London: Methuen.

Steere, E. (1870). *Swahili Tales as Told by The Natives of Zanzibar*. London: Bell & Dadley.

P' Bitek, O. (1973). *Africa's Cultural Revolution*. Nairobi: Heinemann.

Topan, F. (mh.). (1971). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili: Kitabu cha Kwanza.* Nairobi: Oxford.

Topan, F. (mh.). (1977). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili: Kitabu cha Pili.* Nairobi: Oxford.

Velten, C. (1995). *Swahili Prose Texts.* London: Oxford University Press.

Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. (1989). The Use of Allegory in Shabaan Robert's Prose Works. Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-muwa.

Wa Thi'ongo, N. (1986). *Decolonising the Mind.* London: Heinemann.

Wa Thiong'o, N. (1998). *Penpoints, Gunpoints and Dreams*. Oxford: Clarendon.

Werner, A. (1933). *Myths and Legends of Bantu*. London: Frank Cass.

Zubkova, E. B., Gromov, M. D., Khamis, S. A. M. & Wamitila, K. W. (2009). *Outline of Swahili Literature: Prose Fiction and Drama.* Leiden: Brill.